# Jarida la UQAB

**Toleo 7**
**Agosti 2017 MILADI**
**Dhul-Qa'adah 1438 AH**

**Nguzo Zisizo za Kiaskari**

**Desturi za Kihuni na Uislamu**

**Shakhsiya za Watumwa Wawili Watukufu**

**Kupenda/Kuchukia kwa Ajili ya Allah**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 3**

**Kuziondoa Pesa za Haramu na Udanganyifu katika Biashara**




## Tunapinga Kushikwa kwa Wanachama wa Hizb ut-Tahrir Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

# Tunapinga Kushikwa kwa Wanachama wa Hizb ut-Tahrir Kenya

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Siku ya Jumatatu tarehe 3 Julai, 2017, wanachama watatu wa Hizb ut-Tahrir Kenya walifikishwa mahakamani Mombasa kwa mashtaka ya kupeperusha vipeperushi ambavyo havina jina na eneo analoishi mchapishaji na mpeperushaji. Wanachama hao waliofikishwa mahakamani ni:

**Shabani Mwalimu – Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**
**Bakari Mohammed – Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut-Tahrir Kenya**
**Mahmoud Majid – Mwanachama wa Hizb ut-Tahrir Kenya**

Hizb ut-Tahrir Kenya tunakemea kwa kinywa kipana kushikwa kidhulma kwa wanachama wetu na tungependa kusema yafuatayo:

- Tumekuwepo Zaidi ya miaka 20 ndani ya Kenya. Hatujawahi kuhusishwa na masuala yoyote ya uchochezi wa aina yoyote.

- Kazi yetu ndani ya Kenya ni kuwasilisha Uislamu kama suluhisho mbadala katika kutatua matatizo ya wanadamu. Lengo letu kuu likiwa kurudisha maisha ya Uislamu kupitia kusimamisha serikali ya Khilafah ndani ya nchi iliyo na Waislamu wengi. Katika kufikia lengo, tunajifunga kikamilifu na Njia ya Utume na kamwe hatutumii nguvu wala vurugu.

- Tunasema wazi kuwa majanga yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayoshuhudiwa leo ndani ya Kenya na ulimwenguni yanatokamana na ulafi na ufisadi wa mfumo wa kimagharibi wa kirasilimali.

- Tunasisitiza kuwa demokrasia imefeli ndani ya Kenya na ulimwenguni katika kuwaunganisha watu, kudumisha Amani, utulivu na ufanisi. Demokrasia ni nidhamu iliyobuniwa maalumu kuwanufaisha wachache matajiri na sio mtu wa kawaida kama inavyodaiwa. Kura za kidemokrasia ni mashindano kati ya matajiri ili kuchukuwa mamlaka na kujitajirisha. Hivyo basi, wanasiasa wa kidemokrasia wanatumia mbinu zozote kufikia mamlakani na hivi sasa hayo ndiyo yanayoendelea Kenya huku ripoti tayari zikiashiria na kutoa onyo kuwa kuna uwezekano wa vurugu za uchaguzi. Haingii akilini kudai kuwa walinganizi wa kurudi tena kwa mfumo wa Kiislamu kuwa ndio tishio kwa usalama wa taifa na uchaguzi.

Tukimalizia, tunasema tukio hili ni maandishi ya Mola 'Qadhaa' na halitoirudishwa Hizb ut-Tahrir Kenya nyuma au kuitia hofu katika usimamizi wake juu ya mambo ya watu, kuwahesabu viongozi and kufichua maovu ya mfumo wa kirasilimali. Bali, tutasonga mbele na ulinganizi wa kweli huku macho yetu yakiikodolea Khilafah kwa Njia ya Utume ambayo itawakomboa wanadamu wakiwemo wasiokuwa Waislamu ambao hivi sasa wanataabika kwa umasikini, vita, ufisadi na majanga mengineyo yanayosababishwa na mfumo wa kirasiliamali.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Nguzo Zisizo za Kiaskari za Dola ya Kiaskari ya Kiingereza Afrika Mashariki




**1. Kadi ya Kitambulisho cha Kidijitali; Nidhamu ya Gereza la Kijamii Lililodhibitiwa Kuingia ndani yake**

Mpango wa nyumba kumi pamoja na utekelezwaji wa kadi ya kitambulisho cha kidijitali ulio unganishwa ndani ya mfumo wa kamera za uchunguzi za Safaricom utakuwa ni ala ya nguvu ya usimamizi kutokana na kuwa inagusa nyanja zote za maisha ya mtu binafsi. Hii ni kusema kuwa mbali na mwendo, kadi ya kitambulisho cha kidijitali itawezesha kudhibiti miamala yote ya kijamii na kiuchumi ya watu binafsi na jamii kwa jumla.

Na hili wala si chuku, haya ndio maono kama yalivyo tangazwa na serikali ya Kenya yenyewe. (http://www.nation.co.ke/news/State-starts-process-to-issue-Kenyans-with-super-ID/1056-2340886-roykwrz/index.html)

Kudhihirisha sura yake; hivi tuzungumzavyo majumba mengi na taasisi nyingi tayari hakuna ruhusa ya kuyaingia pasi na kadi hizi za utambulisho. Uhalisia wa mfumo huu wa kadi unafanya kuwa vigumu kutekelezwa bila ya kuzingatia gharama zake za kifedha na uwezekano wake.

Kadi hii ya kitambulisho cha kidijitali pamoja na sheria inayozitaka taasisi kuwa na mfumo huu wa kudhibiti uingiaji utawezesha si tu kumchunguza mtu akiwa ndani ya masafa ya mita fulani na kunakili miamala yote pekee (ambalo hili tayari linafanyika) bali pia kumuekea vikwazo mtu binafsi hata katika muamala wa kiwango cha chini kabisa.

Hii ni kusema kuwa, leo huku ikiwa inawezekana kuwachunguza na kuwaandama watu na idadi jumla ya wakaazi, haiwezekani kuwadhibiti au kuwaekea mpaka wa matembezi na miamala.

Lakini kwa kuja kwa kadi ya kitambulisho cha kidijitali na pesa za kidijitali (mfumo wa pesa zisizo taslimu), itawezekana kumfungia mtu binafsi nje ya jamii sio tu kiuchumi bali kimwili pia pindi taasisi zote kijamii na kiuchumi zitakapo idhinisha “chimbuko moja tu la ukweli” muundo mbinu wa kitambulisho cha kidijitali.

Yaani majumba ambayo kwa sasa hivi hatuwezi kuyaingia kwa sababu bawabu ndio ametuzuia kuingia yatakuwa hayaingiliki tena kutokana na milango yake kutofunguka na kuturuhusu kuingia, hii itasambaa mpaka katika nidhamu ya kiuchumi.

Sote tutaishi ndani ya gereza kubwa lililo wazi milango yake, lakini ukiorodheshwa kwa ubaya utakuwa ni mwenye kufungwa kifungo cha nje. Itakuwa inawezekana kufurushwa kutoka katika jamii bila ya kufuatiliwa au kutolewa kivitendo.

Wanaharakati katika magharibi walipinga kisiasa kadi za vitambulisho vya kidijitali kwa kuzinduliwa na hatari yake nayo ni kuwapa uwezo usiokuwa na mipaka watu wasiojulikana juu ya jamii nzima, na serikali ya Amerika haija faulu kutabikisha mfumo huu juu ya raia wake. Hili halijaizuia serikali ya Amerika kuacha kufuatiliwa utabikishwaji wake juu ya jamii nyenginezo kama ilivyo dhihiri katika matangazo ya mwaka wa 2014 ya waziri Ole Lenku na naibu raisi William Ruto baada ya kila ziara ya Amerika, kuwa wanafanya kazi na serikali ya Amerika na Israel kutabikisha mfumo wa kadi ya kitambulisho cha dijitali.

Upinzani huu kwa sasa hauna nguvu, kwani nukta ya kiingilio cha mfumo wa kitambulisho cha kidijitali tayari ishaamuliwa na mabwenyenye wa kiulimwengu kuwa iwe pia ndio mfumo wa fedha, na kutokana na nguvu walizo nazo mabwenyenye hawa zimeufanya upinzani huu kutokuwa na natija yoyote.

*Endelea Uk..4*

Mtazamo huu wa kongamano la kiuchumi la kiulimwengu unafuatwa kwa uaminifu na kutekelezwa na wakala wa humu nchini.

Nukta ya kiingilio ya udhalimu huu wa kidijitali ni mfumo wa fedha na sio wa kisiasa, na utapenya kuwafikia wananchi. Huduma ya M-PESA ambayo ndio muundo mbinu msingi wa muamala wa kifedha kwa watu, unadhihirisha jukwaa la mahusiano la kihakika la mfumo wa kitambulisho cha kidijitali linalounganisha katika ya fedha na mawasiliano ya simu.

Kilicho muhimu kuzingatia hapa sio suala la kujijengea gereza linalo tuzunguka wenyewe, bali ni kumjengea mtu mwengine gereza linalo tuzunguka sisi wenyewe. Wala hii si siri. Edward Snowden atufichulia kuwa hatumiliki simu zetu, kwa sababu sisi hatumiliki barinamiji (software) inayo endesha simu zetu.

Lakini kulingana na gazeti la 'Daily Nation', Bi Gatabaki anatujuza kwa furaha kuwa kifedha hatuumiliki hata huo mfumo wa kitambulisho cha kidijitali yaani tumelipiwa na mtu mwengine asiyejulikana.

Kule kuwa hatumiliki gereza hili la kidijitali katika kiwango chochote kile, si kiufundi wala kifedha ni jambo ambalo sio siri. Bi Gatabaki akafichua kwa watu wote…

Bi Gatabaki alifafanua maumbile yote ya kindani ya mradi huu mzima kwa njia ya kujinaki, "Tutafika wakati ambapo hutaweza kupata huduma msingi za umma pasi na kuwasilisha kitambulisho chako cha kidijitali". Matumizi ya kinyume ya mfumo huu ambayo Bi Gatabaki hayazungumzii ni kule kutumiwa kama njia kutoa 'orodha nyeusi'. Pindi tu utabikishaji wake ukianza, itawezesha kumfungia mtu nje ya mujtamaa kiuchumi na kijamii.

Kile ambacho (Bi Gatabaki) hakioni ni kuwa vile vile itawezesha kumfunga mtu kimwili pia, yaani, sio tu kijamii na kiuchumi pekee.

Kwa sasa hivi Afrika, mfumo wa serikali unatoa huduma chache. Mtazamo mkubwa wa serikali hizi uko katika ukusanyaji. Kwa watu wengi wanaofanya kazi za reja reja (blue-collar jobs), kuwekwa katika orodha nyeusi (na serikali) itakuwa na manufaa sawa kama kupiga msasa 'Sura ya 11' ndani ya Amerika. Mtu ataokoka kutokana na mtoza ushuru na wadeni wote kupitia kuigeuzia njia mbadala miamala yake ya kiuchumi kwa badali ya gharama kiasi fulani kwa jina la 'ada ya muamala' au 'ada ya wakala'. Kile tunachostahili kuelewa ni kuwa orodha hii nyeusi haitajifunga tu katika mazingira ya kiuchumi na ya kiidara kama taarifa ya Bi Gatabaki inavyo jaribu kuashiria, orodha hii nyeusi itakuwa na uwezo wa kumfungia mtu nje kijamii.

Kumbuka jamii imegeuka kufikia nukta ambayo miamala yote hata ya kijamii inatekelezwa kupitia muundo msingi wa kidijitali; sera mpya ni, jamii ya kimtandao.

Itawezekana kikamilifu kuwa mtu aliye wekwa katika orodha nyeusi hatakuwa na uwezo tu wa kufanya mawasiliano na biashara bali hatakuwa na uwezo pia kuingia katika sehemu za umma.

Mfumo wa kadi ya kitambulisho cha kidijitali utawezesha kumfungia mtu kikamilifu katika upeo wa kijamii kwa urahisi kwa kutumia tu kijisanduku cha upekuzi.

Huu ndio uhakika, lengo na uwezo wa mfumo wa kadi ya kitambulisho cha kidijitali, kitovu cha kiteknologia cha serikali ya kiaskari ya Hifadhi ya Kiingereza ya Afrika Mashariki.

**2. Sheria**

i. Agizo la Kiidara Nambari 9066 la 1942

Mpango wa jiji la Nairobi unaoongozwa na Mh. Aden Duale unao lenga kuigeuza Nairobi kuwa eneo la kijeshi una historia nyeusi ya kale na malengo maovu.

Una historia ya kiamerika inayojitokeza kupitia agizo la kiidara nambari 9066 la 1942 lililotiwa sahihi na aliyekuwa raisi wa Amerika Franklin D. Roosevelt linalo idhinisha katika hali ya kivita, makamanda wa kijeshi kutangaza maeneo ya kiamerika kuwa maeneo ya kijeshi ambapo watu wote wanaweza kufukuzwa kutoka maeneo hayo. Agizo hili limetumiwa dhidi ya watu walio na asili ya kizazi kutoka kwa adui wa kigeni.

Kile anachohitaji mtu kufanya ni kuondoa tu neno Amerika na kuweka neno Kenya na watu ambao ni Waislamu/Wasomali ili kuulewa vyema mswada uliopendekezwa na Mh. Aden Duale wa 'Metropolitan Command Initiative Bill'.
Amerika imelifadhili jeshi la Kenya ambalo liko katika hali ya kivita na Somalia, na huenda kwa mfano siku moja ikawaondoa Wasomali wote Nairobi na kuwaweka katika makambi au katika gereza kubwa kama ilivyo fanya serikali ya kiamerika kwa Wajapani siku za nyuma.

Mswada uliopendekeza na Mh. Duale utakuwa ni kama mapinduzi yaliyo endeshwa na bunge, mandhari ya chombo cha kuendesha siasa za kiraia kusalimisha utawala kwa 'khiari' kwa wanajeshi, hali itakayo pelekea jiji hili kuu kuwa chini ya utawala wa kijeshi. Tutakuwa chini ya kanuni za kijeshi kupitia maamuzi yaliyopitishwa na sheria ya kiraia. Ni muhimu kutaja hapa kuwa, hii itakuwa ni kuingia mahali pasipo tokeka tena. Huwezi kulipitishia jeshi kanuni barabarani, kwa msemo wa Kaisari "Alea iacta est", ukiwa na maana kuwa karata hatimaye itachezwa.

Kule kuwa mpango huu unaongozwa na Msomali na Muislamu itaupatia uhalali utakaolipa uwezo jeshi kuwafungia Waislamu na Wasomali. Historia ya uangamizaji unao sababishwa na oparesheni 'Linda Nchi' inapaswa kutoa muongozo wa kutosha wa kiwango cha ghasia ambacho mswada huu utaleta kwa raia hawa walengwa.

*Endelea Uk..5*

ii. Mswada wa Serikali ya Uingereza wa Kupambana na Misimamo Mikali Na Mkataba wa Snooper Aina ya +254

Mapendekezo ya mkuu wa sheria ya kudhibiti taasisi za kidini na mitandao ya kijamii yalikuwa ni jaribio la kuazima sheria moja kwa moja kutoka Uingereza. Jitihada zake zinashabihiana sawia na jitihada za Theresa May kimaneno na kiwakati na mswada wake wa Kupambana na Misimamo Mikali wa 2015 pamoja na mkataba wa Snooper. Kwa bahati nzuri upinzani mkali uliotoka kwa watu wa dini ulipunguza makali ya shambulizi lake dhidi ya watu wake mwenyewe kwa niaba ya ubepari. Watu wa dini walitambua kuwa ufafanuzi wa maana ya misimami mikali na ugaidi haukuwekwa wazi kimakusudi. Hivyo basi lafdhi hizi za 'mtu mwenye misimamo mikali' na 'gaidi' zina weza kutumiwa dhidi ya mtu yeyote au kikundi chochote cha watu katika hali yoyote au wakati wowote ambao watu walio mamlakani wataamua. Hii ndio iliyo pelekea kiongozi wa upinzani Raila Odinga kutuhumiwa na msemaji wa polisi "kueneza fikra hatari…" akinukuu kutoka kwa sheria ya kupambana na ugaidi ya 2012, alipo kusanya watu kuwataka viongozi wa tume ya uchaguzi kujiuzulu. Baadaye, kanuni hizi hizi za kupambana na 'ugaidi' zilitumiwa kuwaweka kizuizini wabunge sita maarufu kama 'Watu sita wa Pangani' na kuwanyima dhamana.

**3. Uchunguzi Unaofanywa na Madikteta (Fascist)**

Sekta ya kibiashara ya kibinafsi inayotekeleza jukumu na kazi ambazo ni za serikali katika usalama na uchunguzi; mradi wa kamera za uchunguzi za Safaricom pamoja na uchunguzi wa mawasiliano ya sauti na data.

**4. Mtazamo**

Mkusanyiko wa yote tuliyo yataja juu hayana ukweli wowote isipokuwa ukaidi tu wa watu na serikali. Licha ya hayo yanaibua maswali mengi muhimu sana. Nguzo za sheria zinaipatia hifadhi ya kisheria serikali ya kiaskari. Vifaa hivi vya kiteknologia vitaupanua uwezo, nguvu na upeo wake kwa kiasi kikubwa sana. Mkusanyiko wa vifaa hivi unaligeuza eneo hili kuwa gereza kubwa la wazi. Unakipatia kikundi cha watu chache sana uwezo wa kuangalia na kudhibiti mienendo ya raia jumla kwa upeo mpana na watu binafsi kwa upeo mdogo katika hali ya umakinifu mkubwa.

Kuna maswali muhimu sana ambayo mabadiliko haya yanaibua. Kuna kadhia muhimu sana ambazo matabaka yote ya jamii yanahitaji kuzifahamu na kujihusisha nazo, kwa sababu kama tutakavyo fichua katika toleo letu lijalo, hatumiliki wala kudhibiti nyanja yoyote katika mfumo huu wa kiutawala wa kimabavu.

Historia yaashiria kuwa hakuna hata mradi mmoja kati ya hii ambao chimbuko lake ni humu nchini. Bi Gatabaki na Ole Lenku walifichua kuwa mradi mzima wa kitambulisho cha kidijitali umefadhiliwa, kumilikiwa na kutekelezwa kutoka ng'ambo lakini hawakufafanua ni nani haswa anaye umiliki na kwa nini na vipi serikali ya Kenya kusalimisha udhalimu na mnyororo huu juu ya shingo za raia wake.
Wabunge wamekosa upeo mpana wa kifikra ndiposa wakapendekeza sheria hizi zenye uovu mkubwa.

Miswada ya kupambana na ugaidi ilipitishwa kwa zaidi ya nchi 100 kwa muda wa chini ya miaka 15.

Ni jambo linalo julikana dhahiri kuwa wabunge humu nchini huweza tu kushirikiana kwa pamoja katika kupitisha marupurupu yao. Hakuna anayeweza kutafakari kuvumilia fikra hii ya Aden Duale kiongozi wa wengi bungeni; fikra ya kutangaza jiji la Nairobi kuwa eneo la kutoa amri za kijeshi. Wala hata kwa makisio madogo haiwezekani kudai kuwa majenerali wa kijeshi humu nchini ndio wanaoshinikiza mradi huu, kwani twatambua kuwa sekta yao (bunge) imepewa lakabu ya "tender-preneurship" yaani watu wanaongazia tu namna gani ya kujishindia kandarasi hata kama ni kwa njia isiyo halali.

Kwa uchache, makataa ya muda wa mapendekezo ya Theresa May kwa mkataba wa Snooper na mkuu wa sheria wa Kenya yanadhihirisha usanii wake.

Ni nani aliye idhamini kampuni ya Safaricom mradi wa upelelezi wa serikali ya Kenya katika wakati ambapo uorodheshaji wa hazina ya mikopo ya S&P ulikuwa wa kutilia shaka? Uorodheshaji wa hazina na serikali ya Kenya haukufuzu kwa ufadhili na uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta ya kibinafsi. Na kuyaamini maneno ya Bob Collymore kwamba Safaricom inaiamini serikali ya Kenya kwa shilingi bilioni 14 ya pesa za wenye hisa wake (ambapo tayari serikali ya Kenya imeanza kulipa faini ya riba ya kiwango cha juu kwa kuchelewa kulipa deni lake, hii ikithibitisha kuwa ni mdeni asiyevutia kamwe) katika maneno yake "kama washika dau ni sharti tuwe washirika katika vita dhidi ya ugaidi…" kwa maana nyengine ni kuwa mtu atakapo dhani kuwa maneno haya yanatokana na uzuri wa moyo wake, anafuzu kuwa bwege.

Haya ndio maswali muhimu. Maswali ambayo tutaendelea kuyaangalia kwa kina, katika matoleo yajayo.

**Arkanuddin Yassin**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano – Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Vijana wa Kiislamu Baina ya Desturi za Kihuni na Uislamu



"**Nyinyi ni umma bora muliotolewa kwa watu munaamrisha mema na munakataza maovu**" [TMQ Aali-Imran: 110]

Allah anatuarifu katika ayah hii ya Qur'an tukufu kuwa sisi ni umma bora tuliotolewa kwa ajili ya wanadamu. Lakini, watu wanapo tazama uhakika wa Waislamu leo na hususan uhakika wa vijana wa kiislamu katika jamii yetu, wanajiuliza maswali, 'Itakuwaje hawa ndio umma bora waliotolewa kwa ajili ya wanadamu?' wanapoona vijana wa kiislamu wakijihusisha na desturi za kihuni na mihadarati, hawaoni isipokuwa mgongano baina ya vile nususi za kisheria zilivyo wasifu na vile walivyo wenyewe kihakika.

Uhalisia wa tatizo hili haupo ndani ya Uislamu bali tatizo linatokana na vijana wa leo wa kiislamu kupoteza muelekeo kutoka katika mizizi yao. Ikiwa tutaangalia historia yetu, tutaona kwa wepesi kuwa hadhara ya kiislamu ilikuwa ndio bora zaidi, yenye maendeleo na mafanikio makubwa zaidi katika zama zote. Ilikuwa ni hadhara iliyo faulu katika nyanja zote za maisha; iwe ni kisiasa, kiuchumi, kijamii au kiroho.

Hadhara ya kiislamu ilikuwa mstari wa mbele ulimwenguni kwa karne kumi na nne na kitovu cha umma huu kilikuwa ni vijana wake. Vijana walikuwa nguzo muhimu katika kusimamisha dini hii na kulifanya neno la Allah kuwa juu zaidi. Kwa masikitiko, baadhi ya vijana wa kiislamu leo wamepoteza muelekeo katika Uislamu na historia ya Uislamu. Wanawafahamu zaidi watu mashuhuri wa kimagharibi, na kuwafanya kiigizo kwao, kuliko wanavyo wafahamu watu mashuhuri zaidi katika historia ya kiislamu, Maswahaba wa Mtume wa Allah (saw) na wema wengine waliofuata baada yao.

Leo kuna makundi kadhaa ya vijana. Kuna wale wanaowaiga wasanii wa nyimbo za kufoka foka (hip-hop) na 'wanaotaka kuwa wahuni', huku wakitembea kwa fahari, wakibadilishana lugha za matusi, wakidhani kuwa ni sawa kwao kutumia mihadarati na kujihusisha na uhalifu. Wengine wako katika kundi la kwenda vilabuni na kufanya uasherati kana kwamba hawata kwenda kuhisabiwa kwa wanayo yafanya. Mahusiano ya kimapenzi baina ya wavulana na wasichana yamekuwa ndio ada ambapo inaonekana kuwa ajabu ikiwa mtu hata toka nje kwa matembezi na mtu wa jinsia ya pili au hata kujaribu tu. Kupoteza muda imekuwa ndio jambo maarufu ambapo muziki, michezo ya tarakilishi (computer games), filamu na kubarizi ndio yamekuwa mambo ya kawaida ya kupotezea muda. Kuwaasi wazazi kumefikia kiwango kipya, ambapo watoto wamefikia kuwa wageni (strangers) kwa wazazi wao wenyewe na kujihisi tulivu zaidi wakiwa na marafiki zao kuliko familia zao. Wanajifunza namna ya kufikiri na kutenda katika njia ilio geni na Uislamu huku wakizidi kujazwa na thaqafa ya kimagharibi kupitia runinga, shule na jamii kwa ujumla.

Kuna mifano mingi kutoka kwa Maswahaba vijana, wanaume na wanawake, waliokuwa ni viongozi katika Uislamu. Mus'ab ibn 'Umayr (ra) alikuwa na umri wa 24 pekee na alitumwa Madina na Mtume wa Allah (saw) kwenda kueneza Uislamu, 'Aisha (ra) mke wa Mtume wa Allah (saw) alikuwa na athari kubwa sana katika kuendeleza na kufafanua Uislamu licha ya umri wake mdogo, Usama ibn Zaid ambaye alikuwa na miaka 17 pekee alipo waongoza Maswahaba wakongwe mfano wa Abubakar (ra) na Umar (ra) kama amiri wao wa jeshi la jihad, Ja'far ibn Abi Twalib ambaye katika umri wa miaka 20 aliweza kusimama katika mahakama ya mfalme Najash wa Habasha na kuwawakilisha na kuwatetea Waislamu kwa ufasaha.

Mbali na hawa, tutambue kuwa watu mashuhuri miongoni mwa vijana waliendelea kuwepo hata baada ya zama za Maswahaba. Imam Shafi, mmoja wa wanazuoni wakubwa wa umma huu, alihifadhi Qur'an akiwa na umri wa miaka 7, na alikuwa mujtahid, mwanachuoni, na wenye uwezo wa kuvua masuluhisho kutoka katika Qur'an na Sunnah akiwa na umri wa miaka 14. Tariq ibn Ziyad mfunguzi wa Andalusia (Spain) na Muhammad al-Fateh, mfunguzi wa Kostantinia (leo yajulikana kama Istanbul), wote walikuwa ni vijana.

Kuna mifano mingi ya vijana wa

*Endelea Uk..7*

kiislamu waliosimama kwa ajili ya Uislamu na wakapata mambo makubwa kwa ajili ya Allah (swt). Jambo muhimu kuzingatia ni kuwa nyuma, chini ya utawala wa kiislamu, hii ilikuwa ni kawaida kwa vijana. Mazingira yalitawaliwa na Uislamu, matukio makuu katika jamii hayakuwa juu ya ni nani anacheza na nani katika mechi ijayo, bali yalikuwa juu ya ni vipi tutakavyo lieneza neno la Allah (swt)?

Hatua za kivitendo zifuatazo ni naswaha kwa vijana wa kiislamu na wale waliopewa jukumu la ulezi wao. Kwa wale ambao hawautekelezi Uislamu, insha'Allah zitawasaidi kuanza kuutekeleza na kwa wale ambao tayari wanautekeleza, insha'Allah zitawasaidia kuimarisha zaidi ibada zetu kwa Allah (swt).

**1) Kujielimisha Juu ya Uislamu**

Mtume wa Allah (saw) asema:"**Kutafuta elimu ni faradhi juu ya kila Muislamu**" [Ibn Majah] Kila mmoja wetu ni lazima adumishe kutafuta elimu kuhusu Uislamu, kwani ndio jambo muhimu zaidi katika maisha. Kwa hivyo ni lazima tujue juu ya imani ya kiislamu na sheria yake.

**2) Kuunganisha Vitendo Vyetu na Matokeo katika Akherah (Kiyama)**

Muislamu ni lazima aunganishe moja kwa moja vitendo vyake na matokeo, malipo na adhabu za akherah. Hana budi kuvuta taswira ya haya kila anapo fikiri kufanya kitendo cha haramu; hisia hii juu ya Allah (swt) na akherah inatakikana iwe ndio ngao ya kutulinda kutokana na madhambi na itushajiishe katika kuvuna thawabu. Ikiwa tutataka kuwaasi wazazi katika jambo la haramu, tutambue kuwa Mtume wa Allah (saw) amezungumzia juu ya hili. Imepokewa kutoka kwa Anas (ra) kwamba Mtume wa Allah (saw) aliulizwa juu ya dhambi kubwa na la kuchukiza. Akajibu (saw): "**Miongoni mwa madhambi makubwa: kumshirikisha Allah, na kuuwa nafsi (pasi na haki), na kuwaasi wazazi wawili (kuwasababishia maumivu au majeraha), na kusema (ushahidi wa) urongo**" [Bukhari]. Ikiwa tuko karibu na kukosa swala, tukumbuke kuwa Mtume wa Allah (saw) amelinganisha kuacha swala na ukafiri. Mtume wa Allah (saw) asema: "**Mkataba uliopo (tofauti) baina yetu na wao ni swala anaye iwacha (kwa makusudi) amekufuru**" [Musnad Ahmad]. Ikiwa tutavutiwa na ulevi kama tembo au mihadarati iwe kwa viwango vidogo au vikubwa, tujitahadharishe na maneno ya Mtume wa Allah (saw). Mtume wa Allah (saw) asema: "**Tembo ni mama wa machafu na mwenye kulinywa Allah hatazikubali swala zake kwa muda wa siku arubaini, na akifa na tumboni mwake muna tembo amekufa kifo cha kijahiliya**"

**3) Kuwa Ndani ya Mazingira Mazuri**

Kubakia ndani ya mazingira sahihi ni muhimu kwa Muislamu ili kuweza kujiepusha na vishawishi vinavyo letwa na Shetani. Aina ya mazingira waliyomo ndani yake baadhi ya vijana wa kiislamu leo ni fisidifu mno yaliyo tawaliwa na mihadarati, ulevi, nyimbo chafu na matangamano huru baina ya wanaume na wanawake. Aghlabu mazungumzo yote huwa ni kuhusu jinsia ya pili, muziki, runinga, filamu, michezo ya tarakilishi na mfano wa haya. Ni nadra sana kuwepo na mazungumzo muhimu katika maisha.
Abu Musa amehadithia kutoka kwa Mtume wa Allah (saw) akisema: "**Mfano wa mfuasi mzuri na mfuasi mbaya ni kama mfano wa muuza manukato na muhunzi wa vyuma; ama muuza manukato huenda ukanunua kutoka kwake manukato au huenda ukapata harufu nzuri kutoka kwake, na muhunzi wa vyuma: ima atazichoma nguo zako au utapata harufu mbaya kutoka kwake.**" [Bukhari Mujalad 3, No 314]. Ni lazima tutambue kwamba marafiki tusuhubianao leo duniani ndio tutakao suhubiana nao akherah. Maana halisi ya urafiki ni kutokubali mwenzio kuukaribia moto wa Jahanam badala yake kusaidiana katika kuikurubia pepo. Mara nyengine wale watu wanaodhania kuwa marafiki zao wa karibu zaidi huenda wakawa ndio maadui zao wabaya zaidi ikiwa wanawasababisha kupata ghadhabu za Allah (swt).

4) Ubebaji Ulinganizi (Da'wah) kwa Wengine

Tunapo usoma Uislamu, tunahitaji pia kuubeba kwa wengine. Mtume wa Allah (saw) asema: "**Nifikishieni kutoka kwangu japo aya moja.**" Maswahaba wengi walianza kuulingania Uislamu punde tu walipo silimu licha ya kuwa walikuwa na elimu chache mno kuuhusu. Kubeba Uislamu kwa wengine, kuamrisha mema na kukataza maovu ni wajib na kwa uhakika ndiko kunako tufanya tuwe makini zaidi katika vitendo vyetu wenyewe.
Ni lazima tutambue kwamba katu hatuwezi kuwa wakamilifu – tutafanya makosa. Uislamu haukuteremshiwa malaika, uliteremshiwa wanadamu.

**5) Kufuata Uislamu haimaanishi Tuwe Marobot**

Baadhi ya watu wana ufahamu wa kimakosa kuwa kufuata Uislamu ina maana kuwa ni lazima ugeuke kuwa robot au kuhani na huna ruhusa ya kupumzika. Uislamu una ruhusu kujipumzisha na kustarehe maadamu tu zinaambatana na sheria na wala hazita tuweka mbali na twa'a ya Allah (swt).
'Aisha (ra), mama wa waumini, ahadithia, "**Mambo matatu ya kidunia yalikuwa yakimstarehesha Mtume wa Allah (swt): chakula, wanawake na manukato. Mawili aliyachukua, lakini moja akaliwacha. Alichukuwa wanawake na manukato lakini sio chakula.**" [Musnad Ahmad]
Mtume wa Allah (saw) alikuwa akipumzika na maswahaba zake na wakeze. Mtume wa Allah (saw) alikuwa hata akiruhusu michezo mbali mbali ya riadha kama kulenga shabaha. Yeye (saw) alisema:"**Jifunzeni kulenga shabaha kwani ndio burudani bora kwenu.**"
Lakini yatupasa tuwe makini kuto athirika zaidi na burudani na starehe

*Endelea Uk..8*

kwani haya huenda yakazifanya nyoyo zetu kuwa ngumu.
Ibn ‘Abbas ahadithia kwamba Mtume wa Allah (saw) amesema:
“**Kuna Baraka mbili ambazo watu wengi huzikosa; afya na faragha ya kufanya kheri.**” [Bukhari]

**6) Uthamini Ujana Wako**

Tunapokuwa vijana tuna uwezo wa kufuata Uislamu kupitia kujiendeleza kiufahamu na kubeba Uislamu kwa wengine. Ujana haubakii milele hivyo basi hatuna budi kuutumia vizuri kabla haujaondoka. Hatuna budi kuhakikisha kwamba tunafuata nyayo za vijana bora wa kiislamu waliotangulia waliokuwa viongozi wa watu. Kumbuka maneno ya Mtume wa Allah (saw) aliposema:
“**Thamini mambo matano kabla mambo matano mengine: ujana kabla ya uzee; afya kabla maradhi; utajiri kabla ya ufukara; faragha kabla ya shughuli; uhai kabla mauti**.” [Tirmidhi]

**7) Jukumu la Wazazi**

Majukumu ya wazazi ya uangalizi na ulezi wa watoto wao yametajwa katika aya kadha wa kadha za Qur’an, vile vile katika hadithi.
Allah (swt) asema: “**Enyi mulioamini, ziokoeni nafsi zenu na za jamaa zenu kutokana na moto (ambao) kuni zake ni watu na mawe…**” [Quran 66:6]

Tutajiokoa vipi na jamaa zetu kutokana na moto huo? Twahitaji kuwaonyesha njia ya sawa na kuwafunza tofauti baina ya usawa na makosa. Mfano mzuri zaidi wa hili ni wasia wa Luqmaan kwa mwanawe, uliopo katika Qur’an, ambapo anamtahadharisha:
a. Kutomshirikisha Allah na kitu chengine
b. Kuwa mwema kwa wazazi
c. Kuwatii wazazi isipokuwa wanapo kuamrisha maovu
d. Kutambua kuwa matendo yetu yote, hata yame madogo kiasi gani, yanaandikwa na yatadhihirishwa kwetu
e. Kudumisha swala
f. Kuamrisha mema na kukataza maovu
g. Kusubiri katika mitihani
h. Kujiepusha na kujifakhiri, dharau na majivuno
i. Kuwa na haya katika tabia na mazungumzo

Huu ndio mfano bora wa jukumu la uzazi na nasaha. Luqmaan anamuongoza mwanawe mwenyewe katika njia ya peponi kwa maneno rahisi lakini yenye ukumbusho.

Watoto ni amana waliopewa wazazi. Wazazi watahisabiwa juu ya amana hii siku ya kiyama. Kimsingi wazazi wana jukumu juu ya akhlaqi, maadili na mafundisho msingi ya kidini kwa watoto wao.

Wazazi wakitimiza jukumu hili, watakuwa huru na matokeo ya siku ya kiyama. Watoto nao watakuwa raia bora na furaha machoni mwa wazazi wao, kwanza hapa duniani, na kesho akherah.

Allah (swt) asema:
((Na wale walio amini na wakafuatwa na vizazi vyao kwa imani tutawakutanisha na vizazi vyao na wala hatuta wapunja hata kidogo katika amali zao...)) [Quran 52:21]

**8) ‘Vikoto’ vya Madrasa**

Ni jambo linalojulikana kwa kila anaye kulia kwenda Madrasa kila siku masaa mawili jioni. Aghlabu badala ya masaa haya mawili kuwa yenye kuleta faida kwa kujaza ufahamu safi na thaqafa ya nguvu ya kiislamu, kwa wengi ni masaa kuogofya – masaa mawili ya kuhifadhishwa huku ukichapwa kwa sababu kadha wa kadha, ikiwemo kosa la kuzungumza darasani na marafiki. Miaka ya utu uzimani marafiki hukumbuka na kucheka kumbukumbu za siku hizi uchungu zilizopita katika madrasa na kulinganisha aina ya adhabu kadha wa kadha ambazo ‘ustadh’ alizitumia, maarufu ya hizo ikiwa ‘kikoto’.


Uhalisia huu unagongana na Uislamu, unatokana na mila zilizo pitwa na wakati na ujinga. Uislamu hauruhusu kupiga watoto kama baadhi leo wanavyopigwa misikitini na madrasa. Mtume wa Allah (saw) kamwe hakupiga watoto wake au wajukuu zake. Alitambulika kama mtu aliye wapenda watoto wake na wajukuu zake, kuongezea, alikuwa mpole sana kwa wajukuu zake wawili Hassan na Hussain, wange cheza mgongoni mwake wakati yuko katika sijda ndani ya swala wala hakuwakaripia. Mtume wa Allah (saw) asema:
“**Wakirimuni watoto wenu na muwalee vizuri. Hakika, watoto wenu ni zawadi kwenu**.” [Ibn Majah]
Uislamu unatambua umuhimu wa elimu kwa watoto. Ibn Majah amehadithia kwamba Mtume wa Allah (saw) amesema:
“**Wasomesheni watoto wenu na muwasomeshe vizuri.**”

Lengo la elimu ni kuunda shakhsiya ya kiislamu katika fikra na tabia. Hili haliwezi kupatikana kwa kuwalazimisha watu kuhifadhi pekee. Bali inahitaji kujenga ufahamu wa mambo msingi katika Uislamu na jinsi ya kuishi kwa kuambatana nayo. Watu hawawezi kugeuzwa kwa fimbo bali kwa kupitia kukinaishwa kikweli na fahamu za kiislamu. Mtume wa Allah (saw) hakuifanya misikiti mahali pa kuchukiza kwenda. Katika zama zake misikiti ilikuwa ndio kituo cha elimu, sio kupiga. Milango ya misikiti ilikuwa wazi kwa vijana kukaa na kujadili kuliko kuwa rasilimali zilizofungwa zinazo endeshwa na kamati kama tunavyo shuhudia leo.

Allah atuongoze njia iliyo nyooka itakayo tupa mafanikio hapa duniani na kesho akherah.

**Fathi Ali Mohammed**

# Kuchukua Mafunzo Kutoka kwa Shakhsiya za Watumwa Wawili Watukufu: Bilal (ra) na Wahshi (ra)



Licha ya muda mrefu kupita, baadhi ya hisia na hatma zinafanana, kwa mfano, hatma na hisia za watumwa hawa kutoka zama za Mtume Muhammad (saw) zinafanana na hatma za baadhi ya watu ambao tabia zao zinalingana na utumwa katika uhakika wa leo. Watumwa wa zamani walitekwa nyara na viongozi wa kiqureishi wenye msemo katika jamii ilhali watumwa wa leo wanatekwa nyara na matarajio, matamanio na udhaifu wao wenyewe nk. Utukufu wa watumwa hawa wawili katika zama za Mtume (saw): Bilal ibn Rabah (ra) na Wahshi ibn Harb (ra) ni ule ambao pia twaweza kuupata katika shakhsiya za Waislamu tofauti tofauti leo.

Watumwa wote wawili wana uhalisia sawa. Wote walitekwa nyara kuwa watumwa, lakini Bilal (ra) alikuwa na mtazamo tofauti kuhusu maisha. Lengo lake daima alikuwa amelielekeza katika kumridhisha Allah (swt) pekee, hata awe katika hali ngumu kiasi gani. Alivumilia mateso mengi kwa ajili ya Allah na kujitolea muhanga sana kwa ajili ya dini yake. Lakini Wahshi hakufurahia hali aliokuwa nayo, alitaka kufanya kila njia kujiweka huru kama wengine. Leo, watu wengi wako zaidi ya Wahshi. Hawaridhishwi na maisha yao na wako tayari kufanya chochote kwa ajili ya mabadiliko pasi na kuzingatia radhi za Allah (swt).

Bilal (ra) hakuwa na ujuzi wa maalum isipokuwa aliweza kutamka Iqama vizuri, leo kila Muislamu anamtambua kwa kujitolea muhanga kwake. Ukweli huu kuwa Bilal (ra) hakurudi nyuma katika Imani yake ya kiislamu na kwamba alipata mateso mengi ulikuwa na athari kubwa kwa Maqureishi zama zile. Tabia hii ilikuwa ni ushindi mkubwa kwa uislamu. Leo, maadui wa uislamu hutumia mbinu za mateso za kisiri na za kuhadaa ambapo japo umma unaona maelfu ya waislamu wakifariki, hili aghalabu halina athari sawa kwao kama tamko 'Ahadun Ahad' kutoka kwa Bilal (ra) mjini Makkah,

Sababu ya hili ni kuwa watu wengi wameshindwa kuutazama huu ulimwengu kama makao ya muda tu ambapo wamo katika vita na shetani. Ikiwa twataka kuwa kama Bilal (ra) hatuna budi kujifunza kufanya kila kitu maishani mwetu kwa ajili ya kumridhisha Allah (swt). Huu ni mtazamo wa maisha uliojaa ikhlas usiokuwa na riyah. Maisha ya watu waliojishughulisha na kumridhisha Allah (swt) pekee hayana chuki, uhasidi, kiburi wala huzuni. Lakini suluki mbaya huwatoa watu katika maana halisi ya maisha na kuwafungulia njia ya moto wa jahanam. Ikiwa mtu anafanya kazi kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah, 'mama wa faradhi zote', ni muhimu pia mtu huyu daima azingatie radhi za Allah (swt) na awe na ikhlas katika mambo yote ya maisha yake. Hii ndio tofauti kubwa baina ya watu hawa wawili. Waislamu leo lazima wachague yupi katika ya watumwa hawa wangependa kumuiga. Zama zimebadilika lakini ujumbe ni ule ule.

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى * وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّى * وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى * إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّى * فَأَمَّا مَن أَعْطَى وَاتَّقَى * وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَى * فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْيُسْرَى * وَأَمَّا مَن بَخِلَ وَاسْتَغْنَى * وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى * فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْعُسْرَى * وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى * إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَى * وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَى * فَأَنذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّى * لَا يَصْلَاهَا إِلَّا الْأَشْقَى * الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّى * وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى * الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّى * وَمَا لِأَحَدٍ عِندَهُ مِن نِّعْمَةٍ تُجْزَى * إِلَّا ابْتِغَاء وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَى * وَلَسَوْفَ يَرْضَى

"Naapa kwa usiku unapo funika* Na mchana unapodhihiri*Na kwa Aliye umba dume na jike*Hakika juhudi zenu bila shaka ni mbali mbali*Ama mwenye kutoa na akamcha Mungu*Na akaliswadiki lililo jema*Tutamsahilishia yawe mepesi*Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja ya wenzake*Na akanusha lililo jema*Tutamsahilishia yawe mazito*Na mali yake yatamfaa nini atakapo kuwa anadidimia? Hakika ni juu yetu kumuonyesha uwongofu*Na hakika ni yetu sisi akhera na dunia*Basi nakuonyeni na moto unaowaka*Hatauingia ila muovu kabisa*Aliye kadhibisha na kupa mgongo*Na mcha Mungu ataepushwa nao*Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa*Na wala si kwa kuwa yuko yeyote aliye mfanyia hisani ndio anamlipa*Ila ni kutaka radhi za Mola wake mlezi aliye juu kabisa*Naye atakuja ridhika"[Surah Al-Layl]

Allah (swt) anataraji kutoka kwa Waislamu suluki fulani; mtu anaye wasaidia wenzake, mtu aliye na uchaji Mungu, na mtu anaye taraji malipo ya mbeleni kutoka kwa Allah (swt) na kamwe hafadhilishi dunia. Allah (swt) atamfanyia njia nyepesi mtu kama huyo ambaye amelenga radhi za Allah (swt). Ili kuwa kama Bilal (ra), yamaanisha kuyafanya haya kuwa ndio tabia yake. Tabia ni muhimu na ni jambo zuri, lakini Muislamu ajishughulishe katika kuwa na tabia njema zinazo mkurubisha kwa Allah (swt). Hivyo basi, ni bora kwa muumini kuwa mtumwa wa Allah (swt) na kupata ukombozi wa milele peponi, kuliko kuwa mtumwa wa dunia hii hadaifu na matamanio yake na kupata kifungo cha milele motoni.

**Amanah Abed**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Kupenda na Kuchukia kwa Ajili ya Allah



Mtume wa Allah (saw) alituongoza katika mizani hii ya kuzidhibiti hisia zetu pindi alipo sema:

(( إِنَّ أَوْثَقَ عُرَى الإِيْمَانِ أَنْ تُحِبَّ فِي اللهِ وَتُبْغِضَ فِي اللهِ ))

"Hakika imani nzito zaidi ni kupenda kwa ajili ya Allah na kuchukia kwa ajili ya Allah."

((يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَن يَرْتَدَّ مِنكُمْ عَن دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ۚ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ )) (المائدة: **54**)

((Enyi Mulioamini! Atakaye iacha miongoni mwenu dini yake, basi Allah atakuja leta watu anao wapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wakali kwa makafiri, wanapigana Jihad katika njia ya Allah wala hawaogopi lawama ya mwenye kulaumu. Hiyo ndio fadhila ya Allah humpa amtakaye. Na Allah ni Mkunjufu na Mjuzi.)) [Al-Maidah: 54]

**((وَالَّذِينَ آمَنُواْ أَشَدُّ حُبًّا لِّلهِ)) (البقرة: 165)**

((Lakini Walioamini wanampenda zaidi Allah [kushinda mwengine yeyote])) [Surah al-Baqarah: 165]

Hadith ya Abu Hurayrah yaeleza kuwa Mtume (saw) amesema: "Watu aina saba watafinikwa na kivuli cha Allah siku ya Qiyama siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa chake Yeye. Nao ni: kiongozi muadilifu, kijana aliye kulia katika ibada ya Allah, mtu ambaye moyo wake umefungamana na misikiti, watu wawili wanaopendana kwa ajili ya Allah, wanashikana kwa sababu Yake na kutengana kwa sababu Yake, mtu anayeitwa na mwanamke mrembo na mwenye cheo kufanya tendo la zinaa naye, kisha akamwambia, 'mimi namuogopa Allah', mtu anayetoa sadaka akaificha mpaka mkono wake wa kushoto usijue mkono wa kulia umetoa nini, na mtu anaye mkumbuka Allah akiwa peke yake mpaka macho yake yakamwaga machozi."

"Kudhihirisha imani ya kuwa hakuna mungu wa haki isipokuwa Allah, yahitaji upende na uchukie kwa ajili ya Allah peke yake, kujenga usuhuba na uadui kwa ajili ya Allah pekee; inahitaji wewe upende kile anachokipenda Allah na uchukie kile anacho kichukia Allah [1] [Ibn Taymiya, al-Ihtijaj bil-Qadar, ukurasa 62]

Ibn Abbas: "Yeyote anaye penda na kuchukia kwa ajili ya Allah, na yeyote anaye funga urafiki na uadui kwa ajili yake Yeye, atapata kutokana na hili, hifadhi ya Allah. Hakuna yeyote atakaye onja ladha ya imani ya kweli isipokuwa kwa kupitia hili, hata kama swala na saumu zake ni nyingi kiasi gani. Kwa hivi sasa watu wamejenga mahusiano kwa ajili ya mambo ya kidunia, lakini hii kamwe haita wanufaisha kwa njia yoyote ile. [1] [Ibn Rajab al-Hanbali, Jami' al-Ulum wal Hikam, ukurasa 30]

Miongoni mwa matendo ambayo yanaonekana kukosekana katika jamii yetu ni "kupendana kwa ajili ya Allah" ambayo inamaanisha kumpenda mja wa Allah kwa sababu ya imani yake na utiifu wake. Licha ya kuwa hili ni jambo muhimu ambalo lapasa kuwamo ndani ya 'nafsiyya' ya Muislamu, leo, wengi wetu hatuonyeshi suluki hii kwa dada zetu na kaka zetu. Tunapo uangalia umma wetu, tutaona kuwa mapenzi haya yametoweka baina yetu. Kwanza, baina ya watu ndani ya familia moja, kisha, baina ya majirani, marafiki na Waislamu duniani. Mwanadamu ni kiumbe cha kijamii aliye na mahusiano mengi na watu wengine. Lakini, mahusiano haya aghlabu huwa yamejengwa juu ya msingi wa faida badala ya radhi za Allah. Tusisahau kuwa "kupenda kwa ajili ya Allah" ni pendekezo kutoka kwa Allah (swt) kama yalivyo maagizo mengine.

Ni kwa nini suluki hii ni muhimu sana? Kuna sababu nyingi na nita nukuu baadhi yake tu. Kwanza, watu wanaopendana kwa ajili ya Allah (swt) ni miongoni mwa aina za watu saba watakao hifadhiwa na kivuli cha Allah siku ya Qiyama. Kisha, katika hadith ya Mtume wa Allah (saw), imetajwa kuwa ikiwa hatuta pendana kwa ajili ya Mungu, basi hatuja muamini Allah kikweli. Tatu, twapaswa kuzingatia malipo ya Allah atakayo tulipa peponi. Ahadi ya Allah (saw) kwa watu hawa ni mimbari za nuru watakao onewa wivu na mitume na mashuhadaa. Kisha, ikiwa tutapendana kwa ajili ya Allah, Allah pia atatupenda.

Baada ya kufahamu umuhimu wa mapenzi haya, tunapaswa basi kufikiria jinsi gani tunaweza kutabikisha amri hii ili ibadilishe suluki yetu.

Kwanza, kwa kumsaidia dada au kaka yetu anapohitajia. Katika njia hii, Ar-Rahman atatuondolea moja ya mazito yetu. Pili, kwa kukutana na wengine kwa uso wa bashasha, Allah huichukulia kuwa sadaqa na kutulipa thawabu kwa hilo. Kisha, kwa kupeana zawadi, hii itaongeza mapenzi tuliyo nayo baina yetu. Kisha, kwa kuwashukuru watu, kwani hili hutia furaha kwa mtendaji jambo, twapaswa pia kumshukuru Al-Kareem, Ar-Rahman. Mengine ni, kukubali msamaha kutoka kwa watu, kuficha siri za watu, kutoa naswaha na kadhalika.

Natamatisha kwa hadith ifuatayo iliyopokewa kwa muafaka (Bukhari na Muslim). An-Nu'man ibn Basheer anaripotia kuwa: Mtume wa Allah (saw) amesema, "Mfano wa Waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao na kuoneana upole kwao, ni kama mfano wa mwili. Kiungo kinapo shitakia maumivu, mwili mzima huitikia kwa kukosa usingizi na homa"



Email: uqab@hizb.or.ke



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 3: Muundo wa Harakati ya Maswahaba (ra)

Mtume (saw) mwanzo wa Da'wah akiwalingania wale ambao anahisi kwao Maandalizi ya Kuikubali hiyo Daa'wah, pasi na kuangalia umri wao, nafasi yao, jinsia yao wala asili yao.

Rasulullah (saw) alikua anawapa Thaqafa wote wanaoingia katika Uislamu juu ya hukmu za dini na kuwahifadhisha quran, na ikafikia idadi ya maswahaba (ra) kutoka kutumilizwa kwake mpaka Allah alipomuamrisha kudhihirisha Da'wah kiasi cha watu arubaini wengi wao wakiwa ni Vijana (Mashabab):

1. Ally Ibn Abiy Twalib - Miaka 8
2. Zubeyr Ibn Awwam - Miaka 8
3. Twalha Ibn Ubaydillah - Miaka11
4. Arqam Ibn Abiy Al-arqam - Miaka 12
5. Abdullah Ibn Mas'ud - Miaka 14
6. Saeed Ibn Zubyr – Chini ya Miaka 20
7. Saa'd Ibn Abiy Waqqas - Miaka 17
8. Suu'd Ibn Rabia'h - Miaka 17
9. Jaa'far Ibn Abiy Twalib - Miaka 18
10. Suhayb Ruumiy - Chini ya Mika 20
11. Zaydu Ibn Harithah - Katika Miaka ya 20
12. Uthman Ibn Affan – Katika Miaka ya 20
13. Tulayb Ibn Umayr - Katika Miaka ya 20
14. Khabab Ibn Aratti - Katika Miaka ya 20
15. Aamir Ibn Fuhayra - Miaka 23
16. Mus'ab Ibn Umayr - Miaka 24
17. Miqdad Ibn Aswad - Miaka 24
18. Abdullah Ibn Jahsh - Miaka 25
19. Umar Ibn Khatwab - Miaka 26
20. Abu Ubaydata Ibn Jaraah - Miaka 27
21. Utbata Ibn Ghazawan - Miaka 27
22. Abu Hudhayfata Ibn Utbah -Katika Miaka ya 30
23. Bilal Ibn Rabaah - Katika Miaka ya 30
24. Ayyash Ibn Rabia'h - Katika Miaka ya 30
25. Aamir Ibn Rabia'h - Katika Miaka ya 30
26. Nua'ym Ibn Abdillah - Katika Miaka ya 30
27. Uthman Ibn Madhu'n - Miaka ya 30
28. Abdullah Ibn Madh'un - Miaka 17
29. Qudaamah Ibn Madh'un - Miaka 19
30. Assaaibu Ibn Madh'un - Miaka ya 30
31. Abu Salamata Al-makhzumiy - Miaka ya 30
32. Abdul rahman Ibnu Awf - Katika miaka ya 30
33. Ammar Ibn Yassir - Kati ya Miaka 30 na 40
34. Abu Bakar Swidiq - Miaka 37
35. Hamza Ibnu Abdul Mutwalib - Miaka 42
36. Ubaydah Ibn Harith - Miaka 50

Itaendelea katika UQAB Toleo la 8…In Shaa Allah.



# SWALI/JAWABU:

## Kuziondoa Pesa za Haramu na Udanganyifu katika Biashara

**Maswali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu Amiri wetu, Allah akupandishe daraja na alete ushindi wa umma huu mikononi mwako.

Nina maswali mawili:

La kwanza: katika jibu lako la swali kwa ndugu yetu kuhusiana na hisa, ulisema: ukimpa mamlaka mamako ambaye ni kafiri kuuzia hisa, ndani ya muda fulani, baada ya kujua kuwa hisa (shares) zimeharamishwa, ni lazima pia uziondoe faida za hisa zako hizo ndani ya muda fulani pia kwa kuzitumia kwa ajili ya maslahi ya Waislamu. Je, kuna dalili gali inayoashiria kuwa azitumie kwa ajili ya maslahi ya Waislamu wakati kisheria yeye siye mmiliki wa pesa hizi, iweje basi aruhusiwe kuzitumia?

La pili: nafanya kazi katika sekta ya uuzaji mboga kama mchuuzi. Nanunua kutoka sokoni ambalo liko umbali wa kilo mita arubaini kutoka mahali nilipo. Baadhi ya wakati hukuta ubovu katika bidhaa… Ni katika desturi kuwa ikiwa mmiliki wa duka la reja reja ataambiwa arudishe bidhaa iliyo haribika ataruhusiwa kurudisha kwa bei chache kuliko alivyo nunulia. Ikiwa nitarudisha bidhaa siku hiyo hiyo, gharama za usafiri zitakuwa juu kuliko hiyo bei. Je, hii ni ridhaa (indemnity) yaani tofauti baina ya bei ya bidhaa zilizo haribika na ambazo hazija haribika? Je, na ile takhfifu (discount) ambayo tunaitisha ni haramu kuichukua?

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu

**Kwanza: Jibu la swali la kwanza kuhusu matumizi ya pesa za haramu:**

1- Yaoneka kana kwamba ulichanganyikiwa na kudhani kuwa maneno yetu: “Ni lazima uziondoe faida za hisa zako katika muda huu wa miezi mitano na uzitumie kwa ajili ya maslahi ya Uislamu na Waislamu” yalimaanisha sadaqa, yaani, kuwa mtu atapata thawabu kwa kuzitumia pesa hizi kwa maslahi ya Waislamu, lakini kadhia sio hivyo, tume sema “ziondoe”, yaani, kama ambaye una vitu visivyo hitajika nyumbani kwako na wataka kuvitoa, bila shaka utaviweka mahali panapo stahili, yaani, hutavichukua vitu hivi na kuvitupa barabarani, na kisha kudai kuwa umeviondoa, badala yake utavichukua na kuviweka mahali panapo stahili, na hii ya maanisha kuwa utachagua mahali panapo faa zaidi kuviweka, au sio? Si itakuwa ni ukosefu wa busara kuvichukua vitu hivi vya ziada na kuvitupa barabarani na kusababisha madhara kwa watu?

Ndio maana tukasema anapaswa kuziondoa faida hizi na kuzitumia kwa maslahi ya Waislamu, na kamwe hapaswi kuzichukua pesa hizi na kwa mfano kuzitupa chini, au kuzitia katika jaa la taka! Ndugu yangu Yusuf, ni lazima aziondoe na kuziweka mahali panapo stahili. Lakini kamwe haita chukuliwa kuwa ni sadaqa kwake na kulipwa thawabu kutokana nayo. Amepokea Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Abdullah Ibn Mas’ood, aliye sema kuwa Mtume wa Allah (saw) amesema:

«وَالذي نفسي بيده...لَا يَكْسِبُ عَبْدٌ مَالًا مِنْ ... حَرَامٍ، فَيُنْفِقَ مِنْهُ فَيُبَارَكَ لَهُ فِيهِ، وَلَا يَتَصَدَّقُ بِهِ فَيُقْبَلَ مِنْهُ، وَلَا يَتْرُكُ خَلْفَ ظَهْرِهِ إِلَّا كَانَ زَادَهُ إِلَى النَّارِ، إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ لَا يَمْحُو السَّيِّئَ بِالسَّيِّئِ، وَلَكِنْ يَمْحُو السَّيِّئَ بِالْحَسَنِ، إِنَّ الْخَبِيثَ لَا يَمْحُو الْخَبِيثَ»

“...Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake… mja hato chuma mali ya haramu kisha akaitumia kisha akabarikiwa kutokana nayo, wala hataitolea sadaqa kisha ikakubaliwa sadaqa yake, wala hato itelekeza (mali hiyo) nyuma ya mgongo wake isipokuwa itakuwa ni zawadi yake ya kumpeleka motoni. Allah ‘azza wa jalla hafuti jambo baya kwa baya, lakini hufuta jambo baya kwa zuri, hakika uovu haufuti uovu.”

2- Kwa taarifa zaidi, imesimuliwa wazi wazi na wanazuoni wa fiqhi kuwa mtu anapaswa kuiondoa mali ya haramu kulingana na sheria. Wame nukuu kama dalili yale yaliosimuliwa kutoka kwa Asim Ibn Kulaib kutoka kwa babake kuhusu bwana mmoja wa kianswari. Alisema: “Tulitoka na Mtume wa Allah kwenda katika mazishi, nikamuona Mtume (saw) katika kaburi akimshauri mchimba kaburi: chimba nafasi kubwa ya sehemu ya miguu na kichwa, aliporudi, alipokewa na mjakazi wa mwanamke, akamletea chakula, kisha akaweka mikono yake juu ya chakula, na watu wakafuata na kula, baba zetu wakamtazama Mtume wa Allah (saw) huku akiendelea kutafuna, Mtume (saw) akasema:

«إني أجد لحم شاة أخذت بغير إذن أهلها»

“Mimi na hisi kutoka katika nyama hii kuwa kondoo huyu alichukuliwa pasi na idhini ya wenyewe”, yule mwanamke akasema: “Ewe Mtume wa Allah, nilimtuma kwa Baqi kuninunulia kondoo lakini hakupata, kwa hivyo nikamtuma kwa jirani

*Endelea Uk..13*

yangu – aliye nunua kondoo – ili aniletee ni mnunue kwa bei yake, lakini hilo halikutokea, nilitumana kwa mke wake, na yeye (mke) akaniletea kondoo huyo, Mtume (saw) akasema:

«أطعميه الأسارى»

“Walishe kondoo huyo mateka” Katika riwaya nyengine, neno lilillo tumika lilikuwa na maana pana zaidi kuliko ‘maslahi ya Waislamu’; walizungumzia kuhusiana na mas’ala jumla ya sehemu ambazo sadaqa inaweza kutumiwa kwa mfano: kuwapa masikini au kujenga misikiti kwa sababu haya ni miongoni mwa mambo ambayo sadaqa yaweza kutumika kwayo. Hii ndio rai ya madh’habu ya Abu Hanifa: Imesimuliwa kutoka katika Hashiyat Ibn ‘Abidin (3/223), na Al-Malik katika Al Jami’ Li Ahkam Al Qur’an na Qurtubi (3/366).

Baadhi ya wanazuoni wamesema “kutumia katika njia ya Allah” maana yake ni “Jihad”. Mmoja kati ya wanaobeba rai hii ni Sheikh Al-Islam Ibn Taymiyah, ambaye amesema katika “Majmoo’ Al-Fatawa (28/401)’, ((Hata kama mtu amepata mali ya haramu mikononi mwake na hakuweza kuiregesha kwa mwenyewe kwa kutomjua, na kadhalika… basi aitumie katika njia ya Allah, hivi ndivyo inavyostahili kutumiwa. Mtu mwenye madhambi mengi tiba yake ni Jihad; na mtu ambaye ataka kujikomboa na haramu na kutubia lakini hana uwezo wa kuirudisha mali kwa wenyewe, basi na aitumie katika njia ya Allah kwa niaba ya wamiliki wake, kwani hii ndio njia ya amali njema itakayo kuwa ndio mkombozi wake kutokana na malipo ya Jihad…)). Na kuna riwaya nyengine nyingi.

**Pili, jibu la swali la pili kuhusu kazi yako ya kuuza mboga, na haya ndio maneno ya swali lako:**

(Nafanya kazi katika sekta ya uuzaji mboga kama mchuuzi. Nanunua kutoka sokoni ambalo liko umbali wa kilo mita arubaini kutoka mahali nilipo. Baadhi ya wakati hukuta ubovu katika bidhaa… Ni katika desturi kuwa ikiwa mmiliki wa duka la reja reja ataambiwa arudishe bidhaa iliyo haribika ataruhusiwa kurudisha kwa bei chache kuliko alivyo nunulia. Ikiwa nitarudisha bidhaa siku hiyo hiyo, gharama za usafiri zitakuwa juu kuliko hiyo bei. Je, hii ni ridhaa (indemnity) yaani tofauti baina ya bei ya bidhaa zilizo haribika na ambazo hazija haribika? Je, na ile takhfifu (discount) ambayo tunaitisha ni haramu kuichukua?) Mwisho wa nukuu.

Jibu lake limefafanuliwa katika (kitabu cha) “**Nidhamu ya Uchumi katika Uislamu” katika sura ya ‘Udanganyifu katika Biashara**’ (Kitabu cha Kiigereza, ukurasa wa 210/ kitabu cha kiarabu, ukurasa 193), kinaeleza:

(… Muislamu haruhusiwi kudanganya katika bidhaa au pesa. Bali anatakikana kuonyesha dosari ilioko katika bidhaa, na kueleza udanganyifu katika pesa. Haruhusiwi kudanganya katika bidhaa kwa lengo la kuisambaza au kuiuza kwa bei ya juu. Wala haruhusiwi kudanganya katika pesa ili ikubalike kama bei ya bidhaa. Hii ni kwa sababu kuharamishwa haya na Mtume (saw) kulikuwa kwa kukatikiwa. Ibn Majah asimulia kutoka kwa ‘Uqbah ibn ‘Amir kwamba Mtume (saw) amesema:

«المسلم أخو المسلم، ولا يحل لمسلم باع من أخيه بيعاً فيه عيب إلاّ بيّنه له»

“Muislamu ni ndugu ya Muislamu, wala si halali kwa Muislamu kununua bidhaa yenye dosari kutoka kwa ndugu yake isipokuwa amuonyeshe dosari hiyo.”

Bukhari pia asimulia kutoka kwa Hakeem ibn Hizam kwamba Mtume (saw) amesema:

«البيّعان بالخيار ما لم يتفرقا، فإن صدقا وبينا بورك لهما في بيعهما، وإن كتما وكذبا محقت بركة بيعهما»

“Wafanyi biashara wawili (muuzaji na mnunuzi) wanakhiari (kutimiza au kuvunja mkataba wa biashara yao) kabla hawaja tengana. Ikiwa walikuwa waaminifu na wakabainisha (bidhaa na pesa) biashara yao itabarikiwa. Lakini ikiwa walificha (dosari) na kudanganya baraka ya biashara yao itaondolewa.”

Mtume (saw) asema: «ليس منا من غش»“Si katika sisi anaye tudanganya (katika biashara)”, kama inavyosimuliwa na Ibn Majah na Abu Dawud kutoka kwa Abu Hurayrah. Yeyote atakaye pata pato kupitia ghushi au udanganyifu haitakuwa milki yake halali (kisheria), kwa sababu udanganyifu sio miongoni mwa njia za kisheria za umilikaji, bali ni katika njia za haramu za umilikaji na kwa hivyo kitu hicho (kilicho patikana kupitia udanganyifu) ni mali ya haramu (Suht). Mtume (saw) asema: «لا يدخل الجنة لحم نبت من سحت، النار أولى به» “Nyama yoyote (mwilini mwa binadamu) iliyo mea kutokana na mali ya haramu (suht) haiingii peponi, moto ndio aula kwa nyama hiyo”, imepokewa na Ahmad kutoka kwa Jabir ibn Abdullah. Ikiwa gushi itatokea kwa bidhaa au pesa, mtu aliye danganywa ana khiari ya kuvunja mkataba au kuendelea nao. Kwa hivyo ikiwa mnunuzi atakhiari kubakia na bidhaa yenye dosari na kuchukua ridhaa, yaani, tofauti ya bei baina ya bidhaa nzima na bidhaa yenye dosari, hana haki ya kufanya hivyo, kwa sababu Mtume (saw) haku ruhusu uchukuaji wa ridhaa (indemnity); bali ilitoa khiari baina ya mambo mawili: «إن شاء أمسك، وإن شاء ردها» “Akipenda aichukue na akipenda airudishe”, kama inavyo simuliwa na Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah.

Kwa hivyo, unapopata dosari katika bidhaa baada ya kuinunua, una khiari ya kuirudisha kwa mwenyewe na kuchukua bei uliyo nunulia, au kuikubali na kubakia nayo… lakini huwezi kubakia nayo kwa kupokea ridhaa kiasi fulani yaani tofauti ya bei kati ya bidhaa nzima na zilizo na dosari. Ama kuhusu masafa marefu yaliyopo kati yako na sokoni unako nunua bidhaa zako, haiathiri hukmu hii. Kama ilivyo katika hadith, una khiari tu ya mambo mawili: «إن شاء أمسك، وإن شاء ردها» “Akipenda aichukue na akipenda airudishe”, kama inavyo simuliwa na Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah.

**Ndugu Yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**15 Shawwal 1438 HIJRI**
**9/7/2017 MILADI**